BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Pili – Tarehe 10 Septemba, 2026
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

187. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inamiliki eneo la ardhi Wilaya ya Bagamoyo.

Je, ardhi hiyo ina ukubwa gani na kwa sasa ipo chini ya mamlaka gani.

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

117. MHESHIMIWA MOHAMMED MANZI HAJI (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kwa muda mrefu, Serikali imeendelea kulitumia eneo la Mwanakwerekwe kwa ajili ya kuzikwa watu waliofariki lakini kwa sasa eneo hili linaonekana kuzidiwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutafuta eneo jengine kwa ajili ya kuzikwa watu waliofariki.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

244. Mheshimiwa Chumu Kombo Khamis (Nafasi za Wanawake): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Ninakipongeza Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kwa kutoa namba za mawasiliano ya haraka, wakati inapotokea ajali maeneo wanayoishi wananchi hasa ajali za moto.

Ni sababu zipi zinazokipelekea Kikosi hicho kuchelewa kufika kwa wakati katika maeneo yaliyopata ajali ya moto.

**Wizara ya Kazi na Uwekezaji:**

232. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Kuna malalamiko ya baadhi ya wafanyakazi hasa wa Sekta Binafsi kuwa, waajiri wao wanawasilisha taarifa tofauti za mishahara yao katika taasisi za Serikali, ikiwemo TRA, kwa ajili ya Payee inayolipwa kwa mujibu wa mshahara wake, ZSSF, michango yake inayotokana na mshahara wake pia na ZHSF kwa ajili ya bima ya Afya. Utararibu huu umekuwa si tu unaikosesha mapato sahihi Serikali, bali pia haki za mfanyakazi kwenye kiwango sahihi cha Hifadhi ya Jamii na Bima ya Afya.

Je, ni lini Serikali itahakikisha taasisi hizi zinaunganisha mifumo yao, ili waweze kubaini udanganyifu huu unaofanywa na waajiri.

**Wizara ya Fedha na Mipango:**

55. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Serikali imekuwa ikitekeleza na kuanzisha miradi mingi ya maendeleo kwa wakati mmoja, ikiwemo miradi mikubwa ya kimkakati inayohitaji rasilimali fedha nyingi, watu wengi na muda wa kutosha. Jambo hili husababisha baadhi ya miradi kuchelewa kukamilika kwa wakati uliopangwa. Ucheleweshaji huu huambatana na kuongezeka kwa gharama za utekelezaji kutokana na mabadiliko ya bei za vifaa na huduma, pamoja na kuchelewesha upatikanaji wa manufaa yaliyokusudiwa kama uzalishaji wa bidhaa, ajira na fursa za kuchochea uchumi.

Kwa nini Serikali haiweki mfumo madhubuti wa kuweka vipaumbele vya miradi, ili kuhakikisha miradi michache yenye tija kubwa inakamilika kwa wakati na kuanza kutoa matokeo kabla ya kuanzisha miradi mengine mipya.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

146. MHESHIMIWA AZA JANUARY JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Tunaipongeza Serikali kwa kuanzisha kilimo cha umwagiliaji maji katika mashamba tofauti nchini ikiwemo, Cheju na Mlemele kwa gharama kubwa sana. Lengo la kufanya hivyo ni kuwasaidia wananchi pamoja na taifa kwa ujumla kuweza kujitegemea kwa chakula.

(a) Je, ni ipi tathmini halisi ya matumizi ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kilimo cha mpunga katika mashamba hayo.

(b) Je, Serikali imenufaika vipi na mradi huu tokea kuanzishwa kwake hadi leo.

**Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:**

299. MHESHIMIWA DKT. NASRA NASSOR OMAR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Kumekuwa na malalamiko kuhusu vifurushi vya data kuisha bila kupata huduma inayolingana, pamoja na intaneti kutofanya kazi, licha ya mwananchi kuwa na kifurushi halali.

(a) Je, Serikali kupitia mamlaka husika, ina mfumo gani wa kufuatilia matumizi na ukataji wa data unaofanywa na kampuni za simu, ili kuhakikisha mwananchi anapata thamani halisi ya kifurushi anachonunua.

(b) Ni hatua gani zinazochukuliwa dhidi ya kampuni za simu pale mwananchi anapokuwa na kifurushi cha data, lakini huduma ya intaneti haipatikani au haifanyi kazi ipasavyo.

(c) Je, kuna utaratibu gani wa kumrejeshea mwananchi data au thamani ya fedha aliyopoteza kutokana na hitilafu ya mtandao ambayo haikusababishwa na yeye.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

139. MHESHIMIWA ABDULGHANI ISMAIL ZUBEIR (Jimbo la Malindi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Naipongeza Serikali kwa kuandaa Mfumo wa Ulinzi wa Kamera za Barabarani kwa lengo la kudhibiti makosa ya barabarani. Hata hivyo, *criminological deterrence theory* inaeleza kwamba, madereva hufuata utii wa sheria pakiwa na uwezekano mkubwa wa kukamatwa wanapofanya makosa kuliko kukiwa na faini kubwa. Kwa kuwa mifumo hii ya kamera inauhakika wa kumpata mfanyaji kosa barabarani kwa asilimia kubwa na kupunguza *enforcement gap*.

Je, Wizara ina mpango gani wa kupunguza faini ya makosa hayo kwa kuwa *enforcement gap* imepungua kwa kutumia mifumo ya kamera za barabarani.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

11. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Sekta ya Uwekezaji ni sekta muhimu sana kwa maendeleo ya Zanzibar pale inapokuwa sheria pamoja na haki zinapokwenda sambamba baina ya Serikali, Mwekezaji na Wananchi wa maeneo yanayolengwa kuekezwa, ili kuepusha kabisa migogoro katika utekelezaji wa miradi hiyo ya uwekezaji.

(a) Je, Serikali inatumia mkabala (approach) gani kuchukua maeneo ya wananchi bila ya taarifa na bila ya kuwalipa fidia na kuwapa wawekezaji.

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani kuzirejesha ardhi hizo kwa wahusika.

(c) Ni upi mpango mkakati wa kuzuia kadhia hizo kisiwani Pemba.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

80. MHESHIMIWA JUMA USONGE HAMAD (Jimbo la Chaani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Tunaishukuru Sekali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa utekelezaji wa ajenda ya Uchumi wa Buluu (Blue Economy). Katika kuitekeleza agenda hiyo, wanawake wengi wa Pwani Mchangani na Kandwi, wamehamasika katika kilimo cha mwani, ingawa wanakabiliwa na changamoto ya athari za mvua, hasa ikizingatiwa kuwa sasa tunaelekea katika msimu huo.

(a) Je, Serikali kupitia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, ina mpango gani wa kujenga makaushio ya mwani katika Shehia ya Pwani Mchangani.

(b) Ni wakulima wangapi wa Jimbo la Chaani wamepatiwa nyezo mbalimbali katika kilimo hiki cha mwani.

## II. HOJA ZA SERIKALI:

### Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kuanzisha Shirika la Magazeti ya Serikali, Nam. 11 ya 2008 na Kutunga Upya Sheria ya Shirika la Magazeti Zanzibar kwa Madhumuni ya Kuendesha Biashara ya Magazeti na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa Mara ya Pili.

**Zanzibar,**
**10 Septemba, 2026.**

**(Ramadhan Khamis Juma)**
**KAIMU KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR**